

❖ **Kuyaishi maisha ya ndoa kabla ya ndoa yenyewe.**

Vijana wengi hujiusisha na mapenzi au ngono kabla hawajaoa au kuolewa hii huwapelekea kuhisi hakuna umuhimu wa kuingia katika ndoa kwasababu mahitaji anayohisi angepata kwenye ndoa tayari anayapata akiwa hajaingia kwenye ndoa. Wasichana na vijana wengi wamekuwa wanajirahisisha sana hawaoni haya kuvua nguo zao na kutoa uchi kwa rafiki zao kabla ya kuingia kwenye ndoa. Kumbuka thamani ya kitu kinaongezeka pale ambapo haujakiona kwasababu unakuwa na kiu ukione. Huyo kijana hawezi kuona jambo geni kwako kwasababu alishakuona uchi wako wala hana hamu na wewe anajaribu kumtafuta mwingine akihisi yamkini atakuwa na utofauti na wewe. Natoa ushauri Kwa vijana wasiingie kwenye mapenzi kabla hawajaoana hiyo itawafanya kila mmoja amuone mwenzie wathamani Sana. Kuna msemu huko mtaani wanasema amelewa pombe ya kuonja. Hivyo kama amelewa pombe yakuonja ujisahau kuwa huyo mtu atanunua nyingine kwa fedha zake. Na hii ndio tabia inalitesa kanisa nan chi nzima kwa vijana wetu.